

# UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Simu: 202-884-1080  
202-939-6125  
Nukushi: 202-797-7408  
Baruapepe: [ubalozi@tanzaniaembassy-us.org](mailto:ubalozi@tanzaniaembassy-us.org)  
Tovuti: [www.tanzaniaembassy-us.org](http://www.tanzaniaembassy-us.org)

1232 22<sup>nd</sup> Street, N.W.,  
WASHINGTON, D. C. 20037.

## TANGAZO

### **HUDUMA ZA KIKONSELI KWA WAOMBAJI WA HATI ZA KUSAFIRIA**

Tunapenda kuwajulisha kuwa huduma za kikonseli kwa waombaji wa hati za kusafiria (Passports) zitaanza kutolewa kwa siku tatu kwa wiki (**Jumatatu, Jumatano na Alhamisi**) kuanzia tarehe 03 Mei, 2021 kwa wale watakaopatiwa miadi. Huduma hizo zitatolewa kuanzia **3:30 asubuhi** hadi **saa 8:00 mchana** na ni kwa ajili ya hatua za kuchukuliwa alama za vidole na picha tu.

Hivyo basi, wale ambao wameshawasilisha maombi yao Ubalozini na kupokea uthibitisho kuwa yamepokelewa wanaweza kuomba miadi sasa kupitia barua pepe [ppappt@tanzaniaembassy-us.org](mailto:ppappt@tanzaniaembassy-us.org) au kwa simu 2028841080.

**Kabla ya mwombaji kuanza safari ya kuja Ubalozini ni lazima kupata uthibitisho wa miadi kwa maandishi na kuwa na nyaraka zote zilizoorodheshwa katika tovuti yetu [www.tanzaniaembassy-us.org](http://www.tanzaniaembassy-us.org).**

Wale ambao bado hawajawasilisha maombi yao waendeleo na utaratibu wa awali wa kujaza fomu kwenye tovuti ya uhamiaji [www.immigration.go.tz](http://www.immigration.go.tz) na kutuma fomu baada ya kupakua na nyaraka zote kwenye barua pepe ya [ubalozi@tanzaniaembassy-us.org](mailto:ubalozi@tanzaniaembassy-us.org).

**UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WASHINGTON DC**

**Aprili 22, 2021**